**LEARNING BY EAR**

# “Mihadarati na vileo – Poromoko la jamii”

## Episode 1: “Maskani”

**Author: Chrispin Mwakideu**

**Editor : Andrea Schmidt, Aboubakary Liongo**

**Proof reader: Charlotte Collins**

**List of characters of episode 1:**

**SCENE ONE : AT LIMBI HIGH SCHOOL**

- **Jabali (m, 18)**
- **Zula (m, 18)**
- **Okosho (m, 18)**
- **Mrs. Chacha (f, 45)**

**SCENE TWO : BAMJU’S ARREST BY INSPECTOR TINO**

- **Bamju (m, 40)**
- **Inspector Tino (m, 40)**

**SCENE THREE: AT MRS. CHACHA'S OFFICE**

- **Jabali (m, 18)**
- **Zula (m, 18)**
- **Okosho (m, 18)**
- **Mrs. Chacha (f, 45)**

## SCENE FOUR: AT CHUNGA SANA POLICE STATION

- **Inspector Tino (m, 40)**
- **Beri (f, 45)**
- **Bamju (m, 40)**
- **Wafungwa 2-4 (m, 16-60)**

**Narrator (m/f)**

**INTRO:**

Nakusalimu mpenzi msilikizaji, na karibu tena katika makala mapya ya “Noa bongo, jenga maisha yako”. Kipindi cha redio ambacho utaweza kujifunza na kuburudika kupitia michezo ya kuigiza. Afrika inazidi kunawiri, nchi nyingi zinapigania demokrasia na kuikumbatia mifumo ya maisha ya kimagharibi. Hayo yanapojiri, kuna changamoto mpya inayoibuka, changamoto ambayo Afrika inaifumbia macho – kama methali ilivyomnadi MBUNI anayekifukia kichwa chake kwenye mchanga asiuone ukweli. Afrika inazidi kupambana na biashara haramu ya mihadarati na vileo. Kuwa nasi katika mfululizo wa vipindi kumi vijavyo, tukiangazia madhara ya mihadarati na vileo barani Afrika , kwa jina **“Poromoko la jamii”.** Tunatabaruku kwa kuwatambulisha waigizaji wakuu katika mchezo huu: Jabali, Okosho na Zula, masahiba hawa watatu wanaishi pamoja katika kitongoji duni. Wamehitimu masomo yao na wamerudi shuleni kuchukuwa majibu ya mitihani. Hapo wanakutana na Bi. Chacha, mwalimu mkuu. Hiki ni kipindi cha kwanza kinachoitwa **“Maskani”.**

## SCENE ONE : AT LIMBI HIGH SCHOOL

1. **SFX: HIGH SCHOOL AMBIENCE (INSIDE)**

**(OKOSHO SINGING A POPULAR SONG, ZULA JOINS IN THE SONG)**

2. **JABALI:** Wewe! Okosho, Zula, wacheni kuimba! Onyesheni heshima tafadhali. Tuko nje ya afisi ya mwalimu mkuu.

3. **OKOSHO:** Heshima?, Upuuzi! Bi. Chacha si mwalimu wangu mkuu tena. Mimi ni mtu mzima sasa. Unajuwa hiyo inamaanisha nini? Eh, Jabali?

4. **JABALI:** Bila shaka nafahamu. Heshima na majukumu.Hayo ndiyo maadili mwalimu alitufunza kuhusu utu-uzima

5. **ZULA:** (**faking Jamaican accent)** Hayo ni mambo ya shuleni, mamen, tukiwa shule. Sisi sio wanafunzi tena. Heshimu Jah pekee yake, man! Rastaman Zula sigopi mtu yeyote, awe mwanamke, au mtoto, kwa taarifa yako…

6. **OKOSHO:** Zula! Ni mara ngapi nimekukanya kuzungumza kwa lahaja hiyo bandia ya kijamaika? Wewe si mmoja wao katu!

7. **SFX: DOOR OPENS. TYPEWRITER SOUNDS IN BACKGROUND**

8. **MRS. CHACHA:** **(loudly)** Mwingine!

9. **OKOSHO:** Nani atatangulia?...Hmm... wewe, Jabali?

10. **JABALI:** Mbona iwe mimi? Zula, nenda wewe kwanza. Si wewe ndio rastaman rui mjamaika.

11. **NARRATOR:** Wakati Jabali, Okosho na Zula, wakijadiliana ni nani ataingia wa kwanza afisini mwa Bi. Chacha kuchukuwa majibu ya mtihani, kule kijijini kwao kulikojulikana kwa jina “ Chunga sana”. Askari walikuwa wamenasa washukiwa wengi. Mmoja wao, alikuwa mwanamume kwa jina Bamju. Tushuhudie kulikoni.

## SCENE TWO : BAMJU'S HIDEOUT IN CHUNGA SANA SLUMS

12.**SFX: HIP-HOP MUSIC PLAYING FROM A PLAYER**

13.**BAMJU:** Starehe ilioje, Kubarizi nyumbani kwako usikilize muziki mzuri, huku ukipulizi moshi taratibu wa kete safi.

14. **SFX: MATCHSTICK BEING LIT. SUBSTANCE INHALED AND SMOKED (STUDIO)**

15.**BAMJU:** Hmm… Ei! Kitu cha nguvu!!!

16.**SFX: MOBILE PHONE RINGING**

17.**BAMJU:** **(answers phone)** Bamju hapa. Oh, Boss! Vyema umenipigia. Lini? Aha. Safi, nitafika hapo. Hamna wasi, siwezi kukubwaga.

18.**SFX: DOOR BANGED HARD**

19.**BAMJU:** Dakika moja, boss, kuna mtu anabisha.

20.**INSP. TINO:** Polisi! Fungua mlango haraka! Bamju, ninajuwa uko! Fungua au nipite na mlango!

21.**BAMJU:** (**in total panic)** Lo! Hapana… nifanyeje? Sitaki kurudi tena jela. Ni lazima nifiche hii bangi…. hapana bora zaidi, nitaitupa nje!!!

22.**SFX: WINDOW QUICKLY OPENED AND THEN CLOSED**

23.**INSP.TINO:** Sawa! Sasa ninavunja mlango. Bamju, ninahesabu mpaka tatu. Moja! Mbili! Tatu!

24.**SFX: WOODEN DOOR BEING HIT SEVERAL TIMES**

25.**BAMJU:** **(loudly)** InspektaTino, watu daima huhesabu mpaka kumi; wewe hutazami michuano ya myereka na masumbwi?

26.**SFX: DOOR SWINGS WIDE OPEN WITH A CRASH**

27.**INSP. TINO:** Kimya. Iko wapi? Eh? Unajuwa ninasikia harufu yake hata ikiwa wapi, na hata wewe pia unaiskia. Kwa hivyo iko wapi, Bamju?

28.**BAMJU:** **(with pride)** Inspekta, yaani si ruhusiwi kutulia nyumbani kwangu? Unaniuliza nini? Umenusa nini? Umesikia harufu yoyote kweli?

29.**INSP. TINO:** Umekuwa ukivuta marijuana. Ni haramu nchini, na unajuwa. Kwa hivyo ninakushika. Lete mikono.

30.**BAMJU:** Unanishika kwa makosa gani tena wakati huu inspekta?

31.**INSP. TINO:** Kwa kuvuta sigara ambayo imeharamishwa! Bangi, cannabis, sativa, marijuana, boza, ile majina yote nyinyi wahuni munaiita!

32.**BAMJU:** Na ushahidi wako uko wapi? Utapeleka harufu kama ushahidi? Hujanishika na bangi.

33.**INSP. TINO:** Usilete mzaha hapa. Hebu fungua mikono, Bamju. Umeficha nini hapo?

34.**BAMJU:** Haya! Huna kesi bwana askari. Sina kitu mikononi. Sikuwa navuta kitu. Labda unabwabwaja, Inspekta.

35.**SFX: JINGLING OF HANDCUFFS**

36.**INSP. TINO:** Uko chini ya ulinzi kwa kupatikana na kutumia vileo haramu. Na chochote utakachofanya au kusema kitatumiwa……

37.**BAMJU** **(finishes sentence): …** Dhidi yangu? Kwanini ni lazima iwe wakati wote ni dhidi yangu? Mbona isiwe dhidi yako?

38.**INSP. TINO:** Kimya! Bamju mahakama ndiyo itamalizana na wewe! Wewe ndiye una hatia, si mimi! Nitaipata tu hiyo bangi, ni lazima iwe iko mahali hapa. Safari hii hauponei ng'oo!

39.**BAMJU:** Unafanya makosa makubwa sana, Inspekta. Makosa makubwa. Hii ngoma hutoweza kuicheza.

40.**NARRATOR:** Uvutaji bangi ni marufuku kwa nchi nyingi za Afrika. Lakini takwimu zinabainisha kuwa ndiyo kileo-moshi kinachotumiwa zaidi. Je, watamshitaki na kumpata na hatia Bamju kwa utumizi wa kileo hicho? Si pinde tutafahamu hayo. Kwa sasa, katika shule ya upili ya Limbi. Zula na Okosho wameshakabidhiwa matokeo yao na Bi. Chacha. Wote wameanguka tifu! Wa mwisho kuingia ni Jabali, na Bi. Chacha hatimae anapata sababu ya kutabasamu.

**SCENE THREE: AT MRS. CHACHA'S OFFICE**

41.**MRS. CHACHA:** Jabali, sote tunafurahia matokeo yako. Kwa niaba ya wafanyikazi wote wa shule hii ya Limbi, nakutakia kila la heri maishani.

42.**JABALI:** **(happy)** Asante sana Mwalimu.

43.**MRS. CHACHA:** Sasa nenda utie bidii na uwe mtu muhimu maishani... usiwache mtu au kitu kikukatize malengo au ndoto yako...

44.**JABALI:** **(cheerful)** Sitokubali. Hata nami nashukuru kwa mafunzo yote muliyonipa hapa shuleni. Sasa nitaweza kujiunga na chuo kizuri. Sina cha kuwalipa ila shukrani. Kwaheri Bi. Chacha.

45.**SFX: DOOR CLOSES. FAINT TYPEWRITER IN BACKGROUND FADES**

46.**OKOSHO:** Ehe? Jabali, umepita mtihani?

47.**JABALI:** **(celebrating)** Nimepita!!!!

48.**ZULA:** Afadhali, mameni. Mimi na Okosho tumeanguka ile mbaya. Angalau mmoja wetu ana akili kichwani, ama vipi?

49.**OKOSHO:** **(unhappy)** Hata hivyo hii karatasi sio muhimu?

| | |
|---|---|
| 50.**SFX:** | **PAPER BEING RIPPED TO PIECES (studio)** |
| 51.**ZULA:** | Miaka kumi na mbili hiyo imepotea bure. Sasa ndio maisha yanaanza mtu wangu, mameni! Mwambie, Okosho! Mueleze! |
| 52.**JABALI:** | **(shocked)** Siamini macho yangu! Umerarua nakala yako ya majibu ya mtihani? |
| 53.**OKOSHO:** | Usijali, Jabali, tuna karamu leo usiku ya wote wale waliomaliza masomo. Nasikia vipusa wa Chunga Sana watahudhuria – mziki mzuri, chakula kizuri. Si unajuwa, kupumzisha akili zetu baada ya mtihani. Utatokea? |
| 54.**JABALI:** | Nikose nichekwe. Iko wapi? |
| 55.**ZULA:** | Kilabu 2000. Mtu wangu! Kuanzia saa nne usiku hadi chee…. |
| 56.**JABALI:** | Ati? Kilabu 2000? Lakini jamaa, licha ya pesa, hatuna hata vitambulisho? |
| 57.**OKOSHO:** | Usijali kuhusu hayo. Saa tatu usiku ikifika wewe uwe ushavaa viatu. Tukutane kituo cha basi! Leo patawaka moto! |

58.**NARRATOR:** Jabali tayari keshapanga msafara wa kuelekea kilabu cha usiku, ijapokuwa yeye, Okosho na Zula  wote hawana vitambulisho, kumaanisha hawapaswi kuingia. Kutatokea nini baadae? Ndio mwanzo mkoko waalika maua. Kwengineko, katika kituo cha polisi, InspektaTino alikua akizozana na afisa muamuru, Bi. Beri, kuhusu kushikwa kwa Bamju. Hebu tujiunge nao tujuwe kunani….

**SCENE FOUR: AT CHUNGA SANA POLICE STATION (Heated argument between Insp. Tino and his commanding officer, Beri)**

59.**INSP. TINO:** (**takes deep breath)** Kumradhi, Afisa mkuu, unasema kwamba…

60.**BERI:** **(authoritative)** Sisemi, Inspekta Tino. **(loudly))** Nina kuamrisha! Nimepigiwa simu kutoka juu na nimekwambia umtoe Bamju kutoka kwa seli haraka!!

61.**INSP. TINO:** Nimemshika akivuta! Huyu mtu ni muhalifu! ninamjuwa, wewe pia unamjuwa… kijiji chote cha Chunga Sana kinamjuwa.

62.**BERI:** (**calmly)** Ninafuata maagizo, na kama unapenda kazi yako fanya hivyo. Jengine ni hili: Utakapomuacha huru, muombe msamaha.

63.**INSP. TINO:** Msamaha?… Wa nini ? Haiwezekani!

64.**BERI:** Inspekta Tino! Hata kama mimi ni mwanamke, lakini mimi ndiye msimamizi hapa! Umeelewa? Muachilie Bamju, na umtake radhi. Sina la ziada.

65.**SFX: Footsteps leaving**

66.**SFX: BUNCH OF KEYS JINGLING. METAL DOOR OPENING**

67.**PRISONERS: MURMURING COMPLAINTS**

68.**INSP. TINO** **(calls out):** Bamju! …Toka uende!!!. **(hushed tone)** sama …sama.. we toke hapa tu...

69.**BAMJU:** **(proudly):** Nilikwambia, Inspekta. Uongo? Nilikwambia ngoma hii ya si ya vijana tena hukusikia.

**OUTRO:**

Inaonekana kuwa Bamju ana marafiki waliyoko katika nafasi za juu serikalini. Lazima kuna mtu mwenye ushawishi aliyemtoa. Inakuwaje katika nchi yenu, mpenzi msilikizaji? Je, ni rahisi kwa walanguzi wa mihadarati kuponyoka mikono ya sheria pia? Je wakaazi wa Chunga Sana,wataathirika vipi kutokana na zali hii na nini kitatokea kwa wale marafiki wetu watatu usiku wa leo katika kilabu cha 2000? Kwa haya na mengine mengi, jiunge nasi katika kipindi kijacho, kuhusiana na mihadarati na vileo vyenginevyo. Kumbuka, ikiwa unataka kukisikiliza tena kipindi hiki au kutuma maoni yako basi tembelea tovuti yetu www.**dw.de/lbe**. mpaka wakati huo – Kwaherini.